

MKATABA WA KUPANGISHA ENEO

Mkataba huu umefanyika leo tarehe ...01..... mwezi wa...09..... Mwaka, 2024

KATI YA

LEAH DAVID..... wa S.L.P 550 Moshi, (ambaye katika mkataba huu atajulikana kama "Mwenye Eneo" neno ambalo litamjumuisha yeye, warithi wake na wote watakaodai haki kutokana na mkataba huu kwa upande mmoja),

NA

Grow King Company LTD wa S.L.P Moshi (ambaye katika mkataba huu anajulikana kama "Mpangaji" neno ambalo litamjumuisha yeye, warithi wake na wote watakaodai haki kutokana na mkataba huu kwa upande wa pili).

KWA KUWA Mwenye Eneo ni mmiliki halali wa Plot No.....70, Block.....KK iliyo eneo la...KATI..... wilaya ya Moshi, mkoa wa Kilimanjoro.

NA KWA KUWA "Mwenye Eneo" ana nia ya kumpangisha "Mpangaji" kwenye eneo hiyo na mpangaji ana nia ya kupanga eneo hilo baada ya kufanya majadiliano baina yao

Hivyo basi mkataba huu unashuhudia haya yafuatayo:-

1. Kwamba "Mwenye Eneo" amekubali mpangaji kupanga Eneo hilo kwa fedha za kitanzania TSH:.....500,000/= katika kipindi cha...MEZI 6.....
2. Kwamba "Mpangaji" atamlipa Mwenye Eneo kiasi cha shilingi TSH:.....3,000,000/=.....katika kipindi chote cha mkataba huu.
3. Kwamba "Mpangaji" ata toa pesa ya tahadhari za kitanzania TSH:.....500,000/= wakati ana weka saini mkataba huu, pesa hizo ni kwaajili ya marekebisho kama mpangaji ata fanya uharibifu wowote kwenye Eneo. Na ata rudishiwa pesa hizo kama kuta kua hamna uharibifu wowote wakati ana ondoka.

4. Kwamba mkataba huu utadumu kwa kipindi cha MTG 6 kuanzia tarehe 01/09/2024 hadi tarehe 01/03/2025 Kodi ya miezi yote italipwa kwa mkupuo siku ya kuweka sahihi mkataba huu.
5. Kwamba **'Mwenye Eneo'** anaweza kufanya ukaguzi wa Eneo hilo kila baada ya miezi miwili kwa kumpa mpangaji taarifa ya kufanya ukaguzi huo katika kipindi kisichopungua siku tatu ambapo ukaguzi huo utafanyika katika majira ya mchana.
6. Kwamba **'Mpangaji'** atawajibika kuweka Eneo lote na mazingira yake katika hali ya usafi kipindi chote cha mkataba na kuhakikisha kuwa eneo inakuwa katika hali ya kukalika muda wote atakao kuwa kwenye mkataba, uharibifu wowote utakaofanywa na mpangaji au jamaa yake atawajibika kuufidia pia mpangaji atawajibika kutunza na kuweka mali ya mwenye Eneo katika hali ya usalama.
7. Kwamba **'Mwenye Eneo'** atawajibika kufanya marekebisho yote katika Eneo hilo ambayo hayatokani na uharibifu wa mpangaji katika kipindi chote cha makataba huu.
8. Kwamba **'Mpangaji'** atalipa kodi ya maji na umeme katika kipindi chote cha upangaji na huduma nyingine atakazokuwa anapata ambazo zinahitaji kulipiwa.
9. Kwamba upande wowote utakaotaka kusitisha mkataba huu utatoa taarifa ya maandishi (Notice) ya mwezi mmoja kabla kwa upande mwingine kabla ya kusitisha mkataba.
9. Kwamba **'Mpangaji'** atatoa tarifa ya nia ya kuendelea na mkataba huu mwezi mmoja kabla ya mkataba kuisha na pande zote zitafanya majadiliano kuhusu mkataba mpya. Kama mpangaji hakutoa taarifa za kuendeleza upangaji wake, itachukuliwa kuwa mpangaji hataki kuendeleza upangaji, hivyo mwenye nyumba atakuwa huru kupangisha mtu mwingine.
10. Kwamba **'Mpangaji'** hataruhusiwa kupangisha nyumba kwa Mtu mwingine au kwa jamaa yake bila idhini ya mwenye nyumba pia mpangaji hataruhusiwa kubadili matumizi ya upangaji bila idhini ya mwenye nyumba.
11. Kwamba **'Mpangaji'** hatawajibika endapo kutakuwa na deni lolote la nyuma katika eneo hilo.

HIVYO BASI, Kwa kuthibitisha hayo yaliyo hapo juu pande zote zimeweka sahihi zao kwa jinsi na tarehe kama inavyosomeka hapo chini.

Umesainiwa na mwenye eneo
leo tarehe 01 Mwezi wa 09 2024



.....
(MWENYE ENEO)

Umesainiwa na mpangaji
leo tarehe 01 Mwezi wa 09 2024



Jina: Rene Kamuis
Tarehe: 1/09/2024
Saini: [Signature]
Cheo: Director

Jina: Jah Albert Den Jong
Tarehe: 1/09/2024
Saini: [Signature]
Cheo: Company Secretary